



Mhe. Lt. Jen. (Mst.) Yacoub H. Mohamed, Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Umoja wa Falme za Kiarabu, leo tarehe 7 Aprili 2026 amewasilisha hati za utambulisho (Credentials) kwa Mheshimiwa Asif Ali Zardai, Rais wa Jamhuri ya Kiislam ya Pakistan katika Ikulu ya nchi hiyo mjini Islamabad.

Mhe. Balozi baada ya kuwasilisha hati hizo alifanya mazungumzo na Mhe. Asif Ali Zardai, Rais wa Jamhuri ya Kiislam ya Pakistan ambapo mazungumzo yao yalijikita katika kuimarisha mahusiano na ushirikiano baina ya nchi za Tanzania na Pakistan.

Hafla hiyo pia ilishuhudia Mabalazi wengine watano kutoka nchi za Ethiopia, Cuba, Spain, Portugal na Singapore wakiwasilisha hati zao za Utambulisho katika Ikulu ya Aiwan-e-Sadr, mjini Islamabad, Pakistan.